Jarida la

# SIHA NA MAENDELEO

UTAWALA BORA

www.sihadc.go.tz | Mwezi Agosti 2024 | Toleo la 18 | Halmashauri ya Siha



# WAZIRI JAFO AWAPONGEZA VIONGOZI KILIMANJARO KWA KUWEKA MAZINGIRA MAZURI YA UWEKEZAJI



*Waziri wa Viwanda na Biashara Mhe. Dkt Selemani Jafo Agosti 23, 2024 alipotembelea eneo la uwekezaji la bustani ya Wanyamapori ya Serval (Serval Wildlife) iliyopo Wilaya ya Siha.*

Waziri wa Viwanda na Biashara Mhe. Dkt Selemani Jafo amewapongeza viongozi wa Mkoa wa Kilimanjaro na Wilaya ya Siha kwa kuhakikisha wanaweka mazingira rafiki na mazuri ya kuratibu uwekezaji katika Mkoa.

Waziri Dkt Jafo ametoa pongezi hizo Agosti 23,2024 alipotembelea eneo la uwekezaji la bustani ya wanyamapori ya Serval (Serval Wildlife) iliyopo Wilaya ya Siha kwa ajili ya kujionea shughuli za uwekezaji katika sekta ya utalii. “Niwapongeze sana viongozi wa Mkoa wa Kilimanjaro na Wilaya ya Siha kwa kuhakikisha wanaweka mazingira mazuri ya kuratibu uwekezaji na kusimamia usalama wa wageni wanapoingia katika maeneo haya ya uwekezaji kwani usalama ni jambo mhimu na sisi Tanzania ni kipaumbele chetu” amesema Mhe Dkt Jafo.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Siha Mhe Dkt Christopher Timbuka amewahimiza wananchi kutumia muda wao wa mapumziko kufanya utalii wa ndani katika bustani hiyo ya Wanyamapori kwa kuona wanyama kwa karibu, kuwagusa na kucheza nao ambao ni jambo tofauti na maeneo mengine ya uhifadhi.

Bustani ya wanyapori ya Serval Wildlife) ni kivutio cha utalii wa wanyamapori na utamaduni kilichopo Wilaya ya Siha Mkoa wa Kilimanjaro ambapo ukiwa katika eneo hilo utakuwa na uwezo wa kuviona vilele vya milima mirefu Barani Afrika Mlima Kilimanjaro na Mlima Meru.






*Waziri wa Viwanda na Biashara Mhe. Dkt Selemani Jafo Agosti 23, 2024 alipotembelea eneo la uwekezaji la bustani ya wanyamapori ya Serval (Serval Wildlife) Kwa ajili ya kujionea shughuli za uwekezaji katika sekta ya utalii uliofanyika katika Wilaya ya Siha.*




*Waziri wa Viwanda na Biashara Mhe. Dkt Selemani Jafo (Katikati) akiwa kwenye picha ya pamoja na Mkuu wa Wilaya ya Siha Mhe. Dkt Christopher Timbuka (kulia) na Mkurugenzi Mtendaji Dkt Haji Mnasi Agosti 23, 2024 alipotembelea eneo la uwekezaji la bustani ya wanyamapori ya Serval (Serval Wildlife).*

## WAWEKEZAJI WA NDANI NA NJE YA NCHI WAKARIBISHWA WILAYA YA SIHA




*Naibu Waziri wa Afya na Mbunge wa Jimbo la Siha Mhe. Dkt Godwin Mollel akiwasilisha wasilisho linaloonesha hali ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwenye Wilaya ya Siha katika kongamano lililofanyika Agosti 04, 2024 katika Ukumbi wa SUMA JKT, Mwenge - Jijiji Dar es alaam alipokutana na wadau wa maendeleo kujadili hali ya ukuaji wa uchumi katika Wilaya ya Siha.*







*Naibu Waziri wa Afya na Mbunge wa Jimbo la Siha Mhe. Dkt Godwin Mollel (Katikati) akiwa kwenye picha ya pamoja na Mkuu wa Wilaya ya Siha Mhe. Dkt Christopher Timbuka (Pili Kushoto), Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha Mhe. Duncan Urassa (Pili kulia), Mkuu wa Jeshi la polisi Wilaya ya Siha - OCD Zakia Shuma (Kwanza kushoto) na Mkurugenzi Mtendaji Dkt Haji Mnasi (Kwanza Kulia) baada ya kongamano lililofanyika agosti 04, 2024 katika Ukumbi wa SUMA JKT, Mwenge - Jijiji Dar es salaam kwa lengo la kujadili hali ya ukuaji wa uchumi wa Siha na Taifa kwa ujumla.*











*Naibu Waziri wa Afya na Mbunge wa Jimbo la Siha Mhe. Dkt Godwin Mollel na Mkurugenzi Mtendaji Dkt Haji Mnasi wakiwasilisha hali ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi katika Wilaya ya Siha kwenye kongamano la Siha Economic Forum lililofanyika Agosti 04, 2024 katika Ukumbi wa SUMA JKT, Mwenge - Jijiji Dar esalaam walipokutana na wadau wa maendeleo kujadili hali ya ukuaji wa uchumi wa Siha na Taifa kwa ujumla.*





*Wadau wa maendeleo wakiwa kwenye kongamano lililofanyika Agosti 04, 2024 katika Ukumbi wa SUMA JKT, Mwenge - Jijiji Dar es salaam kwa lengo la kujadili hali ya ukuaji wa uchumi wa Siha na Taifa kwa ujumla.*

## Dkt. TIMBUKA AFUNGUA MAFUNZO YA JESHI LA AKIBA WILAYA YA SIHA




*Mkuu wa Wilaya ya Siha mhe. Dkt Christopher Timbuka akizungumza wakati wa hafla fupi ya ufunguzi wa mafunzo ya awali ya 14 ya jeshi la akiba iliyofanyika Agosti 15, 2024 kwenye Uwanja wa Isanja Kata ya Nasai.*

Mkuu wa Wilaya ya Siha mhe. Dkt Christopher Timbuka amewapongeza vijana wa Wilaya ya Siha waliojitokeza kupata mafunzo ya awali ya jeshi la akiba kwa uzalendo na kujitolea kutekeleza sheria ya ulinzi ya nchi.

Mhe. Dkt Timbuka ametoa pongezi hizo Agosti 15, 2024 wakati wa hafla fupi ya ufunguzi wa mafunzo ya awali ya 14 ya jeshi la akiba iliyofanyika kwenye uwanja wa Isanja ulipo Kata ya Nasai.

Amewasihi vijana kuzingatia nidhamu na maadili hali itakayosaidia kujenga jamii iliyostaarabika na inayofuata maadili ya Kitanzania.

"Mmemsikia hapa Mshauri wa Jeshi la Akiba Wilaya amesema fani zote zinazohusika na masuala ya ulinzi na usalama wa nchi hii na maadili zitafundishwa, kwa hiyo ni matumaini yangu kwamba mtafuata yale mnayojifunza na mkawe mabalozi wazuri katika jamii" amesema Dkt Timbuka.

Akitoa maelezo mafupi ya mafunzo hayo ya awali ya Jeshi la Akiba Mshauri wa Jeshi la Akiba Wilaya Maj. Tumaini Lukindo amesema vijana 51 wanaohudhuria mafunzo watajifunza mbinu za kivita, ujanja wa porini, usalama wa raia na mali zao, usalama wa taifa, namna ya kuzuia na kuzima moto, namna ya kuzuia na kupambana na rushwa na uhamiaji haramu.

Mafunzo ya awali ya jeshi la akiba yanatolewa kwa vijana wote wa Tanzania wenye umri kuanzia miaka 18 na kuendelea.




*Mkuu wa Wilaya ya Siha Mhe. Dkt Christopher Timbuka na Viongozi wa Kamati ya uasalama Wilaya ya Siha wakiwa kwenye hafla fupi ya ufunguzi wa mafunzo ya awali ya 14 ya jeshi la akiba iliyofanyika Agosti 15, 2024 kwenye Uwanja wa Isanja ulipo Kata ya Nasai.*






*vijana 51 wanaohudhuria mafunzo ya awali ya 14 ya jeshi la akiba wakiwa kwenye hafla fupi ya ufunguzi wa mafunzo hayo kwa Wilaya ya Siha Agosti 15, 2024 yanayofanyika kwenye Uwanja wa Isanja ulipo Kata ya Nasai.*

## MADIWANI SIHA WAFANYA ZIARA YA MAFUNZO WILAYANI TANDAHIMBA MKOA WA MTWARA




*Mkuu wa Wilaya ya Siha Mhe. Dkt Christopher Timbuka, Waheshimiwa Madiwani na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha na Tandahimba wakiwa kwenye picha ya pamoja katika Wilaya ya Tandahimba Mkoani Mtwara.*

Baraza la Waheshimiwa Madiwani Halmashauri ya Wilaya ya Siha Wafanya ziara ya mafunzo katika Wilaya ya Tandahimba Mkoa wa Mtwara Agosti 1, 2024.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha Mhe. Duncan Urassa amesema kuwa lengo la ziara hiyo muhimu ni kujifunza mambo mawili muhimu kuhusu stakabadhi ghalani na uendeshaji wa mfuko wa elimu.

Ameeleza kuwa Halmashauri ya Tandahimba ni Hal mashauri inayofanya vizuri hapa Nchini katika mfuko wa elimu na stakabadhi ghalani ambayo imesaidia Halmashauri ya Tandahimba kuongeza Mapato ya ndani Hadi kufikia shilingi Bilioni 6.7 katika mwaka wa fedha **2023/2024**.

Katika ziara hiyo ya mafunzo Waheshimiwa Madiwani wameambatana na Mhe.Dkt.Christopher Timbuka pamoja na wataalam mbalimbali wa Halmashauri ya Siha akiwemo Mweka Hazina, Afisa Utumishi,Afisa Habari pamoja na Afisa Elimu Sekondari.







*Wah. Madiwani Halmashauri ya Wilaya ya Siha wakiwa kwenye mafunzo Wilayani Tandahimba yenye lengo la kuboresha sekta ya Elimu Msingi na Sekondari kwa kusimamia uendeshaji wa mfuko wa elimu ili uwezeshe miundombinu mashuleni Agosti 2, 2024.*




*Wah. Madiwani Halmashauri ya Wilaya ya Siha wakiwa katika Halmashauri ya Tandahimba katika ziara ya mafunzo muhimu kuhusu stakabadhi Ghalani na mfuko wa elimu Agosti 2, 2024.*

## WATUMISHI WA UMMA SIHA WAPONGEZWA KWA UTOAJI HUDUMA BORA KWA WANANCHI



*Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha* ***Mhe. Duncan Urassa*** *akizungumza kwenye kikao cha Baraza la Waheshimiwa Madiwani kujadili taarifa ya hesabu za mwisho wa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2024 kilichofanyika Agosti 26, 2024 katika ukumbi wa Makao Makuu ya Halmashauri.*

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha Mhe. Duncan Urassa amewapongeza watumishi wa umma katika Halmashauri ya Siha kwa kazi nzuri wanazofanya kuwahudumia wananchi.

Mhe. Urassa ametoa pongezi hizo Agosti 26, 2024 kwenye kikao cha Baraza la Waheshimiwa Madiwani la kujadili taarifa ya hesabu za mwisho wa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2024 kilichofanyika katika ukumbi wa Makao Makuu ya Halmashauri.

Amesema baraza la Waheshimiwa Madiwani linatambua kazi nzuri ya kuwahudumia wananchi inayofanywa na watumishi wa Serikali kuanzia ngazi ya Wilaya hadi Vijiji.

Amewasihi waendelee kufanya kazi kwa ushirikiano na weledi ili shughuli za maendeleo zifanyike na wananchi wa Wilaya ya Siha wanufaike.

“Tunatambua kazi nzuri inayofanywa na Mkurugenzi Mtendaji na watumishi wote ya kuwahudumia wananchi, Katibu Tawala naomba ufikishe salamu za baraza hili kwa Mkuu wa Wilaya ya Siha, kwa kweli anafanya kazi nzuri sana” amesema Mhe Duncan Urassa.

Kikao cha Baraza la Waheshimiwa Madiwani la kujadili taarifa ya hesabu za mwisho wa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2024 ni utekelezaji wa agizo namba 31 (1) la memoranda ya fedha ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2009 inayomtaka Afisa Masuhuli kuandaa na kuwasilisha Hesabu za mwisho kwa Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali.



*Wajumbe na Wataalam wa Mkutano wa Baraza maalum la Waheshimiwa Madiwani la kujadili taarifa ya hesabu za mwisho wa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2024 wakiwa kwenye mkutano Agosti 26, 2024 katika ukumbi wa Makao Makuu ya Halmashauri.*

# WANANCHI JITOKEZENI KUBORESHA TAARIFA KWENYE DAFTARI LA MPIGA KURA – Dkt. Haji Mnasi



*Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha Dkt. Haji M. Mnasi akizungumza kwenye Mkutano wa Baraza la Waheshimiwa Madiwani la kujadili taarifa ya hesabu za mwisho wa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2024 kilichofanyika Agosti 26, 2024 katika ukumbi wa Makao Makuu ya Halmashauri.*

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha Dkt. Haji Mnasi amewaomba Wah. Madiwani na Watendaji wa Kata na Vijiji kuwahamasisha wananchi kujitokeza kwa wingi kuboresha taarifa zao katika daftari la mpiga kura.

Akizungumza Agosti 26, 2024 kwenye mkutano wa Baraza la Waheshimiwa Madiwani la kujadili taarifa ya hesabu za mwisho wa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2024 kilichofanyika katika ukumbi wa Makao Makuu ya Halmashauri.

Dkt. Mnasi amesema wananchi wakijiandikisha na kuboresha taarifa zao kwenye daftari la kudumu na daftari la mkazi la mpiga kura litamwezesha kuchagua viongozi wanaowahitaji.

Amesema zoezi la uandikishaji na uboreshaji wa taarifa kwenye daftari la mkazi na daftari la kudumu la mpiga kura litaanza siku chache zijazo katika Mkoa wa Kilimanjaro, hivyo wananchi wajiandae kujitokeza kwa wingi.

"Tunaendelea kufanya maandalizi wa uboreshaji wa daftari la kudumu la mpiga kura mwezi septemba na uchaguzi wa Serikali za mitaa utafanyika tarehe 27 Novemba 2024 kama ambavyo Waziri mwenye dhamana alitangaza kwa hiyo ipo haja sasa ya kuendelea kuwahamasisha wananchi katika maeneo tunayoyaongoza wajiandae kujiandikisha na kuboresha taarifa zao ili wapate haki yao ya msingi ya kupiga kura" Amesema Dkt Mnasi.

## MAONESHO YA NANENANE
















*Mkuu wa Wilaya ya Siha Mhe. Dkt Christopher Timbuka akikagua na kusaini vitabu vya wageni katika maonesho ya Nanenane Arusha Tarehe 6 Agosti, 2024 yaliyoongozwa na kauli mbiu isemayo, "Chagua Viongozi Bora wa Serikali za Mitaaa kwa Maendeleo endelevu ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi"*









*Waheshimiwa Madiwani Halmashauri ya Wilaya ya Siha wakiwa kwenye viwanja vya maonesho ya Nanenane Njiro Mkoani Arusha* ***tarehe 8 Agosti, 2024****.*

## *DKT MNASI AWAPONGEZA WAFANYABIASHARA KWA KULIPA USHURU NA LESENI ZA BIASHARA MBALIMBALI*




*Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Siha **Dkt. Haji Mnasi** akizungumza na wafanyabishara katika kituo cha mabasi cha KIA Agosti 23, 2024 kwa lengo la kusikiliza changamoto wanazokutana nazo na kuweka mikakati mizuri ya ulipaji wa ushuru na leseni za biashara kwa mujibu wa sheria.*

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha Dkt Haji M. Mnasi amewashukuru wafanyabishara waliopo kituo cha mabasi cha KIA na maeneo mengine ya Wilaya ya Siha kwa kulipa kodi ya vibanda na leseni za biasharakwa mujibu wa sheria.

Akizungumza na wafanyabishara katika kituo cha mabasi cha KIA Agosti 23, 2024 kwa lengo la kusikiliza changamoto wanazokutana nazo na kuweka mikakati mizuri ya ulipaji wa kodi ya pango na leseni za biashara, Dkt Mnasi amesema ushirikiano wanaotoa umewezesha Wilaya ya Siha kuongoza kwa ukusanyaji wa mapato ya ndani kwenye mkoa wa Kilimanjaro.

"Sisi sote tunajua kwamba kodi au mapato ndio agenda namba moja ya nchi, ili tuweze kufanikiwa kuwa na huduma bora za kijamii kwenye maeneo yetu inatulazimu kulipa ushuru kwa wakati, na Serikali yetu inajali sana wananchi wake na tunaamini kwenye ulipaji wa ushuru bila shuruti kwa hiyo tushirikiane" amesema Dkt Mnasi.

"Unapopata changamoto usikae nayo, fika ofisini tutakusikiliza na kukubaliana namna bora ya kutatua changamoto yako, wewe uendelee kufanya biashara na Serikali iendelee kupata mapato kupitia ulipaji wa kodi na leseni za biashara" ameongeza Dkt Mnasi.

Kikao hicho na wafanyabishara ni mwendelezo wa kusikiliza changamoto zinazowakabili wananchi na kuzitafutia ufumbuzi wa haraka ili kufikia adhma ya Serikali ya kutoa huduma bora kwa umma.

***SIHA YAMSHUKURU RAIS KWA KUWAPATIA VITENDEA KAZI MAAFISA KILIMO WA KATA NA VIJIJI***



*Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Siha Dkt Haji Mnasi akimkabidhi vitendea kazi (kishikwambi) Afisa Kilimo wa Kata ya DonyoMurwak ndugu Richard Kabodo wakati wa zoezi la kuwakabidhi vifaa hivyo maafisa kilimo wa Kata na Vijiji lililofanyika makao makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Siha* ***Agosti 16, 2024***

Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Siha **Dkt Haji M. Mnasi** amemshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan kwa kuwapatia vitendea kazi (Vishikwambi na Nguo za kazi) Maafisa kilimo wa Kata na Vijiji ili kuongeza Tija kwa wakulima.

Amesema vifaa hivyo vitarahisisha upatikanaji wa huduma bora za kilimo kwa wananchi na uboreshaji wa taarifa na takwimu zinazotolewa na Halmashauri.

Dkt Mnasi ametoa shukrani hizo Agosti 16, 2024 wakati wa zoezi la kuwakabidhi vifaa hivyo maafisa kilimo wa kata na vijiji lililofanyika makao makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Siha.

Amesema zaidi ya asilimia 95 ya wananchi wa Wilaya ya Siha wanajishughulisha na shughuli za kilimo na ufugaji hivyo kupatikana kwa vitendea kazi hivyo vitawawezesha Maafisa Kilimo kuwafikia na kutoa huduma bora na za kisasa za kilimo kwa wananchi hao.

"Tunaahidi pamoja na maafisa ugani tutaenda kuboresha utendaji kazi kwenye maeneo ya Kata na Vijiji ili kuleta tija kwa wananchi ambapo zaidi ya asilimia 95 wanajishughulisha na kilimo pamoja na ufugaji" amesema Dkt Mnasi.

Katika tukio hilo Mkurugenzi Mtendaji Dkt. Mnasi aliwakabidhi Maofisa kilimo wa Kata na Vijiji Wilaya ya Siha vishikwambi 22 na mavazi maalum ya kazi





*Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Siha Dkt Haji Mnasi (nne kushoto mbele) akiwa na maafisa kilimo wa Kata na Vijiji baada ya kuwakabidhi vitendea kazi (Vishikwambi 22 na mavazi maalum ya kazi) tukio lilifanyika Agosti 16, 2024 makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Siha.*

# HABARI PICHA









*Mkuu wa Wilaya ya Siha mhe. Dkt Christopher Timbuka na Katibu Tawala Wilaya ya Siha mhe. Jane Chalamila Agosti 15, 2024 wakikagua miundombinu ya vyumba vya madarasa katika shule ya Awali na Msingi Suumu Kata ya Kashashi tarafa ya Siha Mashariki .*


# FURSA ZA UTALII WILAYA YA SIHA



***Waziri wa Viwanda na Biashara Mhe.Dkt. Selemani Jafo Agosti 23,2024 alipotembelea Bustani ya kipekee ya Wanyamapori iliyopo Wilaya ya Siha Mkoa wa Kilimanjaro***











**JARIDA MTANDAO LA HALMASHAURI YA WILAYA YA SIHA LIMEANDALIWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI**

**Mkurungenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha**
**5-BR Elerai- Sanya Juu S.L.P 129,25482 siha**
**Simu Na +027-2970677, Nukushi +027-2970677**
**Barua Pepe: ded@sihadc.go.tz, Tovuti: www.sihadc.go.tz**

**Tunapatikana**

Mkurungenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha 5-BR Elerai- Sanya Juu S.L.P 129,25482 siha Simu Na +027-2970677, Nukushi +027-2970677 Barua Pepe: ded@sihadc.go.tz, Tovuti: www.sihadc.go.tz